

Agosti 2008

Kituo cha Mawasiliano cha Wateja: 08456 05 05 05  
Faksi: (+44) 023 8079 2615  
Simu ya maandishi: 023 8079 2906  
(Kwa wale walio viziwi)  
Web: [www.ordnancesurvey.co.uk](http://www.ordnancesurvey.co.uk)

Mtajo wetu: FM7E

Mzazi/Mlezi mpendwa

**Ramani za bure kwa watoto wenye umri wa hadi miaka 11-2008: inayompa mtoto wako ramani za bure ya aina ya Ordnance Survey.**

Leo mtoto wako amepewa ramani ya Explorer™ Ordnance Survey yenye kadiri ya 1:25000 kutoka shule. Ramani hizi zinatolewa kwa wanafunzi wa daraja 7/msingi 7 kwa ajili ya kuwasaidia kusitawisha ujuzi wa kufahamu ramani. Ramani hiyo itakuwa mali ya mtoto wako, na ana haki ya kuimiliki.

Wakati mwingine walimu watawaambia watoto walete ramani zao shuleni. Zitatumiwa katika masomo ya jiografia, kwa kuwa ufahamu wa ramani ni sehemu ya masomo ya shuleni nchini, lakini pengine zitatumiwa katika shughuli nyingine pia. Kwa wingi shule zimetoea ramani za kudhihirisha sehemu za ujirani wa shuleni ama po pote pengine panapotembelewa na watoto kwa kawaida. Watoto wengi watakuwa na bahati nzuri kama sehemu zote mbili za nyumba na shule zipo katika ramani moja.

Kwa ajili ya kujifahamisha ujuzi wa kutumia ramani, watoto wamepewa kijitabu kitiwacho *usomaji wa ramani kwa rahisi na starehe*, (*Map reading made easy peasy*), ambacho kimetayarishwa maalum kwa watoto. Mwaka huu tunaandaa mashindano ya kuwapatia watoto nafasi ya kutembelea mahali pamoja na Kundi la Faragha. Kama mtoto wako angependa kushiriki katika mashindano haya, lazima umpe ruhusa yako na kuweka saini fomu ya kiingilio.

Unaweza kumsaidia mtoto wako kusitawisha ujuzi wa kusoma ramani kwa maswali ya kukuonyesha mahali kwenye ramani na kuthibitisha ujuzi wao wa kutumia wakati wanapotembea nje.

Shukurani kwa kumsaidia mtoto wako kujifahamisha ujuzi wa ramani i ya bure.

Nakala za barua hii zinapatikana kutoka kwa tovuti ya Ramani za Bure (Free maps) katika lugha 10, tafadhali angalia sehemu ya FAQ kwenye tovuti kwa habari zaidi.

Wako mwaminifu,



**Roger Jeans**  
Msimamizi wa Masomo